Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
(Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org

Kwa hakika somo hili ni kubwa na lenye kwenda kwa undani zaidi, lakini kwa ajili ya wasomaji, .tunawaleteeni habari hizi kwa kifupi ili kuwafaidisha

Katika lugha ya Kiarabu, mtu anayeripoti riwaya huitwa ***Rawi*** na sifa zake zimeelezwa na kubainishwa :na *Ma'ulamaa* walio mabingwa wa ilimu ya *Ahadith*

.1 *Rawi* lazima awe mtu mwenye akili na fahamu timamu. Riwaya zozote zitakazotolewa katika hali ya .kuwehuka au kurukwa na fahamu, basi hazitathaminika au kukubalika

.2 Ni lazima *Rawi* awe amebaleghe na awe *Mukallaf*, yaani hukmu za Dini ziwe zimeshakwisha kuwa faradhi juu yake. Hapa inawajumuisha pia vijana wale wote ambao bado hawaja baleghe lakini wanaweza kutofautisha baina ya wema na ubaya. Aina ya vijana hao huitwa *Mumayyiz* na hivyo riwaya .zao zinapotimia masharti mengineyo, huweza kukubalika na kusadikika

.3 .Ni lazima *Rawi* awe Mwislamu. Riwaya za mtu asiye Mwislamu haziwezi kuaminiwa au kusadikiwa

.4 *Rawi* lazima awe ni Mwislamu mfuasi wa *Madhehebu ya Sh'iah Ithna-Asheria*. Lakini iwapo kutakuwa na riwaya kutokea Mwislamu mfuasi wa Madhehebu mengine, itabidi kuangaliwa kwa uzito wa dalili .zinginezo na kufanya uchunguzi iwapo huyo *Rawi* ni mtu aaminiwaye katika historia

.5 Uadilifu wa Rawi pia ni sharti mojawapo, yaani asiwe akifanya madhambi makuu (*Kabair Dhanb*)1 na (wala asiwe akirudiarudia madhambi madogo madogo (*Dhanb-i-Saghirah*)(*al-sagha'ir*

Sheikh Tusi a.r. ametilia mkazo swala hili kwa kuelezea kuwa kuna tofauti katika uadilifu wa *Rawi* na mtoa ushahidi. Iwapo *Rawi* ni *fasiki* na iwapo itathibitika kuwa yeye katika riwaya yake na habari zake ni .mkweli bila ya udanganyifu, basi riwaya yake inaweza kufuatwa

.6 Rawi asiwe msahaulivu, bali awe ni mtu mwenye kukumbuka vyema na udhibiti wake, (yaani haimaanishi kuwa *Rawi* asiwe akisahau kama mtu wa kawaida) yaani *Rawi* anapotaka kuelezea riwaya .au *Hadith*, basi asiwe na mushkeli wa kuikumbuka

.1 Mimi ninatarjumu baadhi ya vitabu ,kama inavyoonekana katika fahiristi hapo nyuma ya kitabu hiki, zinazozungumzia .madhambi mbalimbali

Source URL:
https://www.al-islam.org/ar/kutoa-au-kuomba-sadaka-shaykh-hurr-al-aamili/mwenye-kuripoti-ahadith-aweje